

## **SEHEMU YA KUMI NA TANO**

### **UKAAJI NDANI YA BUNGE**

**116. Mbunge yeyote anayo haki ya kukalia kiti chochote ndani ya Bunge. Hata hivyo, kwa madhumuni ya kurahisisha mawasiliano miongoni mwa Wabunge wa Kambi ya Chama Tawala na pia miongoni mwa Wabunge wa Vyama vya Upinzani, Spika aweza kuweka utaratibu mwingine wa ukaaji wa Wabunge ndani ya Bunge, kadri atakavyoona inafaa, bila kuathiri mpangilio ufuatao:-**

- (1) Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni atakaa kiti cha kwanza akifuatiwa na Mawaziri, upande wa kulia wa Spika. Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni
- (2) Kiongozi wa Upinzani Bungeni atakaa kiti cha kwanza akifuatiwa na Wasemaji Wakuu wa Upinzani upande wa kushoto wa Spika. Isipokuwa kwamba endapo hakuna Kiongozi wa Upinzani aliyechaguliwa kwa mujibu wa Kanuni ya 11 ya Kanuni hizi, lakini Wabunge wa Upinzani wapo, basi Wabunge hao watatengewa sehemu ya kukaa Bungeni kama Spika atakavyoelekeza. Kiongozi wa Upinzani Bungeni na
- (3) Wapambe wa Bunge, Wahudumu wa Bunge, Watumishi wa Serikali wenye shughuli maalum Bungeni na Waandishi wa Vyombo vya Habari watakaa sehemu ambazo zimetengwa kwa ajili yao. Watumishi wa Bunge
- (4) Wageni wa Wabunge, Mabalozi na Viongozi wengine waweza kutengewa sehemu maalum ya kukaa. Wageni